



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Tatu – Tarehe 17 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu kwa mwaka 2024/2025.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu kwa Mwaka 2024/2025.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

158. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) -
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili
wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi walio wengi juu ya kucheleweshwa kupatikana hati za kusafiria (Passport), jambo ambalo linawakosesha haki ya msingi ya kusafiri.

- (a) Je, ni tatizo gani linalopelekea kuchelewa kupatikana kwa hati hizi za kusafiria.
- (b) Ofisi za Uhamiaji zilizopo Wilayani zinasaidia vipi upatikanaji wa hati hizi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

223. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:
- (a) Ni taasisi ngapi zisizo za kiserikali zimesajiliwa kihalali hadi kufikia leo.
 - (b) Ni taasisi gani kati ya hizo ambazo zina malengo mahsusi ya kuulinda na kuudumisha utamaduni wa Mzanzibari.
 - (c) Tathmini ikoje juu ya uwezo na michango inayotolewa na taasisi za ndani ya nchi katika kuisaidia Serikali kupitia malengo ya usajili wao.

Wizara ya Afya:

6. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, tathmini iko vipi juu ya ushiriki wa wanaume katika huduma za afya ya uzazi pamoja na huduma za uzazi wa mpango.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

72. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwa kuwa skuli nyingi za zamani ziko katika hali isiyoridhisha ikiwemo skuli ya Kengeja.

- (a) Je, Wizara yako imejipanga vipi kujenga skuli nyengine

katika eneo hilo.

- (b) Kwa kuwa skuli ya msingi Kengeja inavuja, Je, Wizara yako inalifahamu vipi suala hilo na hatua gani za ziada imezichukua ili kuondosha tatizo hilo.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

58. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nane imefanya kazi kubwa ya kuimarisha michezo nchini na kutokana na kazi hiyo nzuri, baadhi ya michezo kama vile riadha, kuogelea, vinyoya, mpira wa mikono, mpira wa pete, mpira wa vikapu na michezo mengine imeanza kurejea na kupata muamko mkubwa.

- (a) Je, ni upi mpango wa Wizara katika kuongeza nguvu ya michezo hiyo.
- (b) Kwa kuwa katika sherehe za kitaifa kama vile Sherehe za Mapinduzi kunakuwa na hamasa kubwa katika mchezo wa mpira wa miguu, je, Wizara yako imejipanga vipi kuongeza hamasa kwenye michezo mengine mbali mbali.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
17 Mei, 2024.


(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA